# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI UNDOMO
S.L.P 170
NZEGA
TAREHE 11/12/2020.

JINA LA MWANAFUNZI ..........................................................................
SHULE YA MSINGI ATOKAYO....................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UNDOMO HALMASHAURI YA MJI NZEGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021/2022**

**1.0. Utangulizi.**

Ninafurahi kukupongeza na kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

Mhula wa kuanza masomo unaanza tarehe11/01/ 2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe11/01/ 2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 21/01/ 2021 ndani ya siku kumi (10) tu.

**2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia ;-**

**2.1.** Sare za shule .

a) Sare za shule hii ni rangi ya **zambarau**, kwa suruali na sketi kitambaa kizito (2), shati jeupe mikono mifupi (2), viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba na visiwe vya kuchongoka na visiwe na visigino virefu na soksi nyeupe nzito.
Maeleo ya mshono **suruali** isiwe modo na iwekwe marinda mawili (isiwe ya kubana)
b) Tai ya **zambarau**
c) Tisheti rangi ya zambarau yenye nembo ya shule **ITAVALIWA JUMATANO NA IJUMAA TU.**
d) Sweta la **zambarau** kwa ajili ya baridi
e) Mkanda mweusi kwa ajili ya suruali wavulana
f) Sare ya michezo **ni jezi kamili rangi ya bluu** kwa wavulana na kwa wasichana ni **track suti rangi ya zambarau**
g) Kwa wasichana sketi rangi ya **zambarau** isiwe **rinda box** na iwe ndefu ya kuvuka magoti, kwa waislamu hijabu iwe nyeupe.

**2.2. Vifaa vya taaluma.**

Daftari kaunta book Q2 tisa (9), kalamu za kutosha za wino wa bluu na nyeusi, penseli HB, rula nzito nyeupe na mkebe wa hesabu.

**2.3. Vifaa vya usafi kilimo.**

Aje na jembe na mpini wake, fagio la nje na ndani pamoja na ndoo ndogo moja (lita kumi)

**2.4.** Faili moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za wanafunzi yaani spring file **(faili la plastiki)**

**3.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule inaendesha kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote nchini na Ofisi ya waziri mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakia kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi katika shule hii.
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare kamili ya shle wakati wote unapotakiwa kuwepo shuleni.
g) Kutokwenda nje na mipaka ya shule bila ruhusa kwa siku zote za masomo
h) Kuhudhuria vipindi vyote vya darasani bila kukosa.
i) Kushiriki shughuli zote za darasani nan je ya darasa kwa mujibu wa ratiba ya shule.
j) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
k) Kutunza mali za shule
l) Mwanafunzi wa kidato cha kwanza anatakiwa kupanda mti atakao utunza hadi anapomaliza kidato cha nne na ataukabidhi uongozi wa shule
m) Kumbuka kuja na vifaavya usafi kama vile, ufagio nan doo ambavyo vitakuwa mali ya mwanafunzi mwenyewe.

**3.1. Makosa yafutayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uongo au umbeya
c) Otoro
d) Kutohudhuria vipindi vya ndani ya darasa nan je ya darasa kikamilifu
e) Uasherati na ushoga
f) Ubakaji
g) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi kubeli na kadhalika.

h) Kupigana na kupiga
i) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
j) Kudharau bendera ya taifa
k) Kusababisha ujauzito
l) Kuwa mjamzito/kupata mimba
m) Kuoa/ kuolewa
n) Kutoa mimba
o) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
p) Kukataa adhabu kwa makusudi.
q) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilisha na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mgamga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakapo ripoti shuleni
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0. Tafahali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu mzazi aje na mwanaye wakati wa kuripoti shuleni**

**6.0. Kumbuka kumpatia mtoto elimu ni lazima. Hivyo mtoto akishindwa kuripoti kwa wakati hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi/mlezi atayeshindwa kuleta mtoto wake kwa wakati shuleni.**

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII**

..........................................

**MWL. MSOMA M. JUMA**
**MKUU WA SHULE**
**0787 849 302**

HEADMASTER
UNDOMO SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 170
NZEGA.